

Je, mbegu za kiume zinaweza kupita kwenye kondomu?

By SW - Melkisedeck Shine · April 16, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Hapana, mbegu za kiume haziwezi kupita kwenye kondomu. Kondomu zimetengenezwa ili kuzuia mbegu za kiume kufikia ukeni wakati wa kujamiiiana. Kwa sababu shahawa haziwezi kupita kwenye kondomu, kondomu ni njia nzuri ya kuzuia mimba pamoja na maambukizi ya magonjwa ya zinaa pamoja na maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Watu wengine wanasema kwamba kuna mashimo madogo kwenye kondomu yanayorahisisha mbegu pamoja na vijidudu vya magonjwa ya zinaa kupita. Huu ni uongo. Ukitaka kuwa na uhakika kwamba kondomu mpya haina mashimo, chukua kondomu moja na ijaze maji ya kawaida. Utaona kwamba maji hayapiti kwenye kondomu kabisa. Baada ya kujaribisha itupe kondomu ndani ya choo cha shimo au ichome moto, lakini usitumie wakati wa kujamiiiana

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25747>